TANGAZO LA SERIKALI NA. 780 la tarehe 30/8/ 2024

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kanuni ya 121(a) na (f))*

# KANUNI ZA UWINDAJI WA KITALII ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
### UTARATIBU WA MAOMBI NA UGAWAJI WA KITALU

3. Utengaji wa vitalu vya uwindaji.
4. Vigezo vya kutenga kitalu cha uwindaji.
5. Upangaji wa madaraja ya vitalu vya uwindaji.
6. Kipindi cha umiliki wa kitalu cha uwindaji.
7. Kugawa kitalu cha uwindaji.
8. Utaratibu wa mnada wa kielektroniki wa kitalu cha uwindaji.
9. Utangazaji wa vitalu vya uwindaji.

### SEHEMU TATU
### MASHARTI NA MAZUIO KUHUSIANA NA VITALU VYA UWINDAJI

10. Ada ya kitalu.
11. Kamati ya ushauri ya mgao wa wanyamapori.
12. Utoaji wa mgao wa wanyamapori.
13. Maombi ya kibali cha utalii wa uwindaji.
14. Mtazamaji.
15. Masharti ya utalii wa uwindaji.
16. Ombi la kufutwa kibali cha uwindaji.
17. Kibali kitakachorejeshwa.
18. Ada ya mnyamapori.

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

19. Matumizi na udhibiti wa mgao wa wanyamapori.
20. Mchango kwa jamii.
21. Tathmini ya utendaji wa kampuni ya uwindaji.
22. Masharti ya kuhamisha kitalu cha uwindaji.
23. Kurejesha kitalu cha uwindaji.
24. Kufutwa kwa umiliki.
25. Mamlaka ya afisa mwidhiniwa.
26. Leseni ya mwindaji bingwa.
27. Usafirishaji wa nyara nje ya nchi.

SEHEMU NNE
MASHARTI YA JUMLA

28. Kosa la kukiuka kiwango kilichowekwa.
29. Adhabu ya jumla.
30. Rufaa.
31. Kufutwa.

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

SHERIA YA UHIFADHI WA WANYAMAPORI,
(SURA YA 283)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kanuni ya 121(a) na (f))*

KANUNI ZA UWINDAJI WA KITALII ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina 1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Utalii wa Uwindaji za Mwaka 2024.

Tafsiri 2. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada ya kitalu" maana yake ni kiasi cha fedha kinacholipwa kwa ajili ya pango la kitalu cha uwindaji;

"ada ya mnyama" maana yake ni bei ya mnyama aliyewindwa au kujeruhiwa na mtalii wa uwindaji;

"ada ya mtazamaji" maana yake ni kiasi cha fedha kinacholipwa na mtazamaji kupitia kampuni ya uwindaji kutazama shughuli za uwindaji;

"ada ya mwindaji bingwa" maana yake ni kiasi cha fedha kinacholipwa na mwindaji bingwa kwa madhumuni ya kumruhusu kuongoza mtalii wa uwindaji nchini;

"ada ya uhifadhi" maana yake ni kiasi cha fedha kinacholipwa na mteja wa uwindaji kwa siku za ziada zilizotumiwa katika kitalu cha uwindaji;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni ile iliyotafsiriwa chini ya Sheria;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania;

"Jumuiya iliyoidhinishwa" itakuwa na maana sawa na iliyotafsiriwa chini ya Sheria;

"kampuni ya uwindaji" maana yake ni kampuni ya biashara iliyosajiliwa, kutengewa kitalu cha uwindaji na Waziri na kupewa cheti cha kufanya shughuli za utalii wa uwindaji;

"kifurushi cha safari" maana yake ni orodha ya wanyama watakaowindwa na idadi ya siku zilizoainishwa katika safari ya uwindaji;

"kitalu cha uwindaji" maana yake ni eneo lenye wanyamapori ambalo limeainishwa au kutengwa na kuthibitishwa na Mkurugenzi kwa ajili ya Utalii wa Uwindaji;

"leseni ya mwindaji bingwa" maana yake ni leseni inayotolewa kwa mwindaji bingwa baada ya kukidhi matakwa ya sheria;

Sura ya 283 "Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Wanyamapori aliyeteuliwa chini ya Sheria;

"mtazamaji" maana yake ni mtu anayefuatana na mtalii wa uwindaji katika safari ya uwindaji kwa lengo la utazamaji tu na hashiriki katika kuwinda;

"mwindaji bingwa" maana yake mtu anayemiliki leseni halali ya mwindaji bingwa inayomruhusu kumwongoza mtalii wa uwindaji;

"safari ya uwindaji" maana yake ni safari inayofanywa na mtalii wa uwindaji kwa ajili ya uwindaji wa wanyamapori katika kipindi cha mapumziko;

Sura ya 283 "Sheria" maana yake niSheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;

"utalii wa uwindaji" maana yake ni uwindaji wa kuchagua mnyamapori ndani ya kitalu cha uwindaji kwa ajili ya burudani au kupata nyara na inajumuisha uwindaji

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

wa michezo na utalii wa uvuvi;

"uwindaji wa nyara" maana yake ni uwindaji wa kuchagua mnyamapori kwa ajili ya pembe, pembe ya ndovu, jino la ngiri au nguruwe, mfupa, kucha, kwato, ngozi, nyama, nywele, manyoya au sehemu yoyote ya mnyama;

"wanyama muhimu" maana yake ni orodha maalum ya reptilia, mamalia na ndege; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na wanyamapori.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA MAOMBI NA UGAWAJI WA KITALU CHA UWINDAJI

Utengaji wa vitalu vya uwindaji

3.-(1) Mkurugenzi atatenga maeneo katika Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, na maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za wanyamapori na maeneo mengine nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kuwa vitalu vya uwindaji na atatoa cheti kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Utengaji wa vitalu vya uwindaji katika Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori utazingatia Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali wa Kanda au Mpango wa Usimamizi wa Jumla wa Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori husika.

(3) Mkurugenzi kabla ya kutenga kitalu cha uwindaji katika eneo lilio nje ya maeneo ya Hifadhi atashauriana na mamlaka ya eneo husika.

Vigezo vya kutenga kitalu cha uwindaji

4. Ikiwa Mkurugenzi anakusudia kutenga kitalu cha uwindaji katika eneo fulani, atazingatia kuwa eneo linalopendekezwa linakidhi vigezo vifuatavyo:

(a) uwepo wa rasilimali za wanyamapori kwa ajili ya utalii wa uwindaji endelevu;
(b) uwepo wa aina mbalimbali za spishi za wanyamapori na makazi yao;
(c) linafikika kwa maana ya muonekano wa eneo na maendeleo ya miundombinu;
(d) uwezekano wa kurejea kwa wanyamapori baada ya uwekezaji kwa muda fulani;
(e) mipaka ya kitalu cha uwindaji kinachopendekezwa kimewekwa mipaka ya majira nukta ya *Global Positioning System* na kuelezwa kwa alama za sura ya nchi au alama za kudumu zinazoonekana kadri inavyoweza kutumia; na
(f) ukubwa wa eneo ni kilomita za mraba 200 isipokuwa ikiwa kitalu cha uwindaji kimetengwa ndani ya Eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ambalo ukubwa wake utaamuliwa katika Mpango wa Usimamizi wa Jumla au Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali wa Kanda kadri inavyoweza kuwa, na kwamba ukubwa wa juu wa eneo utaamuliwa na matokeo ya eneo kwa mijibu wa vigezo vilivyoainishwa katika kanuni hii.

Upangaji wa madaraja ya vitalu vya uwindaji

5.-(1) Mkurugenzi atapanga madaraja ya vitalu vilivyotengwa katika kanuni ndogo ya (3) kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Pili.

(2) Mkurugenzi atapanga vitalu vya uwindaji katika madaraja matatu kwa mujibu wa matokeo ya Daraja la Wastani wa Alama ya kila kitalu yaliyokokotolewa kutokana na vigezo vilivyoainishwa katika Sehemu B ya Jedwali la Pili kama ifuatavyo:

(a) Daraja la I litajumuisha vitalu vya uwindaji vyenye matokeo ya Daraja la Wastani wa Alama kuanzia 3.1 hadi 3.6;
(b) Daraja la II litajumuisha vitalu vya uwindaji vyenye matokeo ya Daraja la Wastani wa Alama kuanzia 2.4 hadi 3.0; na
(c) Daraja la III litajumuisha vitalu vya uwindaji vyenye matokeo ya Daraja la

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

Wastani wa Alama kuanzia 1.7 hadi 2.3.

Kipindi cha umiliki wa kitalu cha uwindaji

6.-(1) Muda wa umiliki wa kitalu cha uwindaji utakuwa kama ifuatavyo:

(a) ikiwa ni kitalu cha daraja la i, miaka kumi;

(b) ikiwa ni kitalu cha daraja la ii, miaka kumi; na

(c) ikiwa ni kitalu cha daraja la iii, miaka kumi na tano.

(2) Muda wa umiliki wa kitalu cha uwindaji kilichoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1), utaanza tarehe ya utolewaji wa cheti cha ugawaji wa kitalu cha uwindaji.

(3) Kampuni ya uwindaji itaacha kufanya shughuli na kuachia kitalu cha uwindaji mwishoni mwa muda wa umiliki.

Kugawa kitalu cha uwindaji

7. Waziri baada ya kupokea ushauri wa Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindajiiliyoanzishwa chini ya Sheria, atagawa kitalu cha uwindaji kwa mwombaji kwa kutumia mnada wa kielektroniki au zabuni.

Utaratibu wa mnada wa kielektroniki wa kitalu cha uwindaji

8.-(1) Waziri atatangaza vitalu vya uwindaji vilivyowazi na kuwaalika waombaji kushiriki katika mnada wa kielektroniki kwa kuchapisha maelezo ya kitalu cha uwindaji pamoja na sifa za waombaji wanaostahili kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi.

(2) Makampuni ya uwindaji yanayotarajia kushiriki katika mnada wa kielektroniki yatatakiwa ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya tangazo, kufanya maombi kwa njia ya kieletroniki kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(3) Baada ya kumalizika kipindi cha maombi, Mkurugenzi kwa idhini ya Waziri atafungua mnada wa kilektroniki wa kitalu cha uwindaji ambao utadumu kwa siku saba tangu ufunguliwe.

(4) Baada ya kufungwa kwa mnadaMkurugenzi atatoa matokeokwa makampuni ya uwindaji yaliyoshiriki mnada na kuitaka kampuniiliyoshinda kulipa malipo ya awali ya asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu ndani ya siku mbili za kazi.

(5) Baada ya malipo ya awali chini ya kanuni ndogo(4) Mkurugenzi atafanya uhakiki wa kampuni ya uwindajiiliyoshinda kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(6) Baada ya uhakiki, Mkurugenzi atawasilisha taarifa ya mnada wa kielektroniki pamoja na mapendekezo yake katika Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji kwa ajili ya mapitio na kumshauri Waziri.

(7) Waziri anaweza, baada ya kuzingatia ushauri uliotolewa chini ya kanuni ndogo ya (6)-

(a) kukubali mapendezo na kutoa barua ya tuzo kwa kampuni ya uwindaji iliyoshinda kitalu cha uwindaji yenye masharti ya kulipa asilimia sabini na tano iliyobakia ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya barua hiyo; au

(b) kukataa mapendekezo na kutoa taarifa kwa kampuni ya uwindaji iliyoshinda na kutoa sababu ya uamuzi huo.

(8) Endapo kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya kwanzaimelipa kiasi kilichobaki cha asilimia sabini na tano ya bei ya mnada-

(a) Mkurugenzi na kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya kwanza watasaini mkataba kwa lengo la kutumia rasilimali za wanyamapori; na

(b) Waziri atatoa Cheti cha Ugawaji wa Kitalu cha Uwindaji kwa namna ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(9) Endapo kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya kwanza itashindwa kulipa asilimia sabini na tano ndani ya siku kumi na nne kama ulivyoainishwa katika kanuni ndogo ya 7(a), Waziri anaweza-

(a) kufuta barua ya tuzo ya kitalu cha uwindaji; na

(b) kutorudisha asilimia ishirini na tano iliyokwisha kulipwa;

(c) kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi kutangaza upya mnada husika ikiwa hakuna kampuni aliyofikia bei ya kitalu; au

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

(d) kuidhinisha utoaji wa kitalu kwa kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya pili na kufikia bei ya kitalu yenye masharti ya kulipa-

(i) asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu ndani ya siku mbili za kazi; na

(ii) asilimia sabini na tano iliyobakia italipwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya malipo ya asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu.

(10) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (9) Waziri atatoa barua ya tuzo kwa kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya pili iliyofikia bei ya kitalu baada ya kulipa asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu.

(11) Endapo kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya kwanza itashindwa kulipa asilimia ishirini na tano ndani ya siku mbili za kazi, Waziri anaweza-

(a) kuifungia kutoshiriki mnada wa kitalu cha uwindaji kwa miaka mitano; na

(b) kumuorodhesha katika rejista ya waharibifu wa zoezi la mnada.

(12) Endapo katika mnada huo, hakuna kampuni iliyofikia bei ya kitalu, Waziri atatoa maelekezo kwa Mkurugenzi kutangaza upya mnada husika.

(13) Endapo kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya pili ilifikia bei ya kitalu, Waziri ataidhinisha kitalu hicho kwa kampuni iliyoshinda mnada nafasi ya pili kwa masharti ya kulipa-

(i) asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu ndani ya siku mbili za kazi; na

(ii) asilimia sabini na tano iliyobakia italipwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya malipo ya asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu.

(14) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (13) Waziri atatoa barua ya tuzo kwa kampuni ya uwindaji iliyoshinda mnada nafasi ya pili iliyofikia bei ya kitalu baada ya kulipa asilimia ishirini na tano ya bei ya kitalu cha uindaji.

Utaratibu wa zabuni kwa vitalu vya uwindaji

9.-(1) Mkurugenzi atatangaza kitalu cha uwindaji kilicho wazi na kualika waombaji kuomba kitalu kwa njia ya zabuni.

(2) Kabla ya kutangaza vitalu vya uwindaji vilivyo wazi, Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindajiitapendekeza thamani ya soko ya vitalu hivyo kwa ajili ya kuidhinishwa na Waziri.

(3) Tangazo litaainisha muda na mahali ambapo waombaji watawasilisha maombi yao.

(4) Maombi ya kitalu cha uwindaji chini ya kanuni ndogo ya (1) yatafanyika kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(5) Mkurugenzi ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea maombi yoyote, atayasajili na kukiri kuyapokea.

(6) Mkurugenzi atawasilisha maombi yote aliyopokea kwa Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji iliyoanzishwa chini ya Sheria kwa ajili ya kujiridhisha na sifa za waombaji na kumshauri Waziri kugawa kitalu cha uwindaji kwa kampuni yenye bei ya juu zaidi ambayo ni sawa au zaidi ya thamani ya soko.

(7) Waziri, baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji, anaweza kuidhinisha bei ya zabuni ya juu zaidi iliyopendekezwa na Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji.

(8) Baada ya idhini ya Waziri, Mkurugenzi atawasilisha maamuzi ya Waziri kwa waombaji na kumtaka muombaji aliyeshinda kulipa bei ya kitalu iliyoidhinishwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe alipowasilisha maamuzi kwa waombaji hao.

(9) Baada ya malipo kamili ya bei ya kitalu-

(a) Mkurugenzi na mshindi wa zabuni watasaini mkataba kwa lengo la kutumia rasilimali za wanyamapori; na

(b) Waziri atatoa Cheti cha Ugawaji wa Kitalu cha Uwindaji kwa namna ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Sifa za kupewa

10.-(1) Mtu hatapewa kitalu cha uwindaji isipokuwa ni kampuni iliyosajiliwa Tanzania na mojawapo ya malengo yake ni utalii wa uwindaji.

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

kitalu cha uwindaji na uhakiki wa mwombaji

(2) Maombi yaliyofanywa chini ya kanuni za 8 na 9 yatawasilishwa kwa Mkurugenzi yakiambatishwa na-

(a) katiba ya Kampuni ya Utalii wa Uwindaji;
(b) cheti cha usajili wa kampuni;
(c) cheti cha utambulisho wa mlipa kodi au namba ya usajili wa kodi ya ongezeko la thamani;
(d) cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi;
(e) ada ya maombi isiyorejeshwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne na nyaraka nyingine kama itakavyoainishwa kwenye tangazo.

(3) Katika uhakiki wa mwombaji chini ya kanuni za 8 na 9, Mkurugenzi atazingatia yafuatayo:

(a) kampuni ina angalau mwajiriwa mmoja mwandamizi katika ngazi ya utawala mwenye elimu na uzoefu wa miaka mitatu katika uhifadhi wa wanyamapori Tanzania;
(b) kampuni inakidhi kiwango cha chini cha hisa na masharti mengine kama ilivyoainishwa katika Sheria;
(c) andiko la biashara likionyesha maelezo ya biashara, muundo wa utumishi, mtaji, wateja wanaolengwa, masoko, mchanganuo wa fedha na matarajio ya mapato;
(d) kumbukumbu nzuri kuhusiana na ulipaji wa ada na uzingatiaji wa Sheria kwa waendeshaji waliopo;
(e) sifa nzuri kutoka kwa mdhamini na kumbukumbu safi za biashara;
(f) kumbukumbu safi za uzingatiaji ulipaji wa kodi ya Serikali na malipo mengine ya kisheria;
(g) ikiwa ni kampuni ya uwindaji inayomilikwa na watanzania, uthibitisho wa-
    (i) eneo la ofisi linalofaa kuendesha biashara ya uwindaji;
    (ii) magari aina ya pick up yenye 4WD yasiyopungua mawili yenye hali nzuri, yaliyosajiliwa kwa jina la kampuni na kukaguliwa na mamlaka husika;
    (iii) uthibitisho wa vifaa vya mawasiliano vyenye kuaminika;
    (iv) angalau mahema sita;
    (v) majokofu mawili na friji mbili; na
    (vi) vitanda na samani zingine za lazima:

Isipokuwa kwamba, kampuni mwombaji inaweza kuwasilisha Dhamana ya Benki au udhamini wa kiasi cha shilingi milioni mia nne badala ya vifaa vilivyoainishwa katika aya ya (h) kama uthibitisho wa kununua vifaa ndani ya miezi mitatu baada ya kupewa kitalu cha uwindaji.

(h) ikiwa ni kampuni ya uwindaji ya kigeni au kampuni ambayo haimilikiwi kwa asilimia 100 na raia wa watanzania uthibitisho wa-
    (i) eneo la ofisi linalofaa kwa kuendesha biashara ya uwindaji;
    (ii) kuwa biashara imesajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania;
    (iii) magari ya *pick up* yenye *4WD* yasiyopungua matano yaliyo katika hali nzuri, yamesajiliwa kwa jina la kampuni na kukaguliwa na mamlaka husika;
    (iv) vifaa vya mawasiliano vya kuaminika;
    (v) angalau mahema kumi na mbili;
    (vi) majokofu matano na friji tano; na
    (vii) vitanda na samani zingine za muhimu:

Isipokuwa kwamba, kampuni muombaji inaweza kuwasilisha Dhamana ya Benki au udhamini wa kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia nne badala ya vifaa hapo juu kama uthibitisho wa kununua vifaa ndani ya miezi mitatu baada ya kupewa kitalu cha uwindaji.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo (1), Mkurugenzi, akilazimika na kwa

madhumuni ya kuthibitisha nyaraka, anaweza kumtaka muombaji kuwasilisha nakala halisi za nyaraka zilizorejewa katika kanuni ndogo (1).

SEHEMU TATU

MASHARTI NA MAZUIO KUHUSIANA NA VITALU VYA UWINDAJI

Ada ya kitalu

11.-(1) Ada ya kitalu cha uwindaji itakuwa-

(a) kiwango cha juu cha fedha ikiwa ni kitalu cha uwindaji kilichotolewa kwa njia ya mnada wa kielektroniki; na
(b) kiwango cha mwisho kilichokubalika na Kamati ya Ugawaji wa Vitalu au Jumuiya iliyoidhinishwa ikiwa kitalu cha uwindaji kimetolewa kwa njia ya zabuni au kwa njia nyingine ya ushindani.

(2) Ada ya kitalu iliyorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) italipwa kila mwaka kabla au tarehe ya kukabidhiwa kitalu cha uwindaji.

(3) Ikiwa mtu anashindwa kulipa ada ya kitalu iliyoainishwa katika kanuni ndogo (1)-

(a) atalipa malipo ya ziada ya asilimia tano juu ya ada ya kitalu; na
(b) hatoruhusiwa kufanya shughuli yoyote ya uwindaji katika kitalu cha uwindaji;

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (3) kampuni ya uwindaji itakayoshindwa kulipa ada ya kitalu kwa miezi minne cheti chake cha kupewa kitalu kitafutwa.

Kamati ya Ushauri ya Mgao wa Wanyamapori

12.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Ushauri ya Mgao wa Wanyamapori ambayo itamshauri Mkurugenzi upangaji wa mgao wa wanyamapori na mapitio ya mgao ya wanyamapori.

(2) Kamati itajumuisha wajumbe saba wafuatao wenye elimu na ujuzi katika masuala yanayohusu usimamizi wa wanyamapori, ambao wanateuliwa na Waziri:

(a) Mwenyekiti;
(b) Afisa mwandamizi kutoka Idara ya Wanyamapori;
(c) Afisa mtafiti mwandamizi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania;
(d) Afisa mwandamizi kutoka Hifadhi ya Taifa Tanzania;
(e) Afisa mwandamizi kutoka Mamlaka ya Uhifadhi ya Eneo la Ngorongoro; na
(f) wawakilishi wawili kutoka Taasisi ya Elimu ya juu Idara ya Wanyamapori au Zoolojia.

(3) Mkuu wa Idara ya Utalii na Huduma za Biashara kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania atakuwa Katibu wa Kamati.

(4) Mjumbe wa Kamati atahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu isipokuwa kama ataondolewa kwenye nafasi hiyo na atakuwa na sifa za kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Utoaji wa mgao wa wanyamapori

13.-(1) Mkurugenzi kwakushauriana na Kamati ya Ushauri ya Mgao wa Wanyamapori, ataweka kiwango cha chini cha mgao wa wanyamapori katika kitalu cha uwindaji kwa mwaka husika.

(2) Mkurugenzi baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Kamati ya Ushauri ya Mgao wa Wanyamapori atatoa mgao wa wanyamapori watakaowindwa kwa kila kampuni ya uwindaji kabla ya msimu wa uwindaji kuanza.

(3) Kampuni ya uwindaji-

(a) haitapunguza mgao wa wanyamapori iliyoidhinishiwa baada ya kuanza shughuli za uwindaji; au
(b) haitazidisha kiasi cha mgao wa wanyamapori ulioidhinishiwa katika kitalu

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

husika.

Maombi ya kibali cha utalii wa uwindaji

14.-(1) Mtu hatafanya shughuli za utalii wa uwindaji isipokuwa kama amepata kibali cha utalii wa uwindaji kutoka kwa Mkurugenzi.

(2) Maombi ya kibali cha utalii wa uwindaji yaliyorejewa chini ya kanuni ndogo (1) yatafanywa kwa kutumia Fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tano.

(3) Iwapo Mkurugenzi ataridhia maombi yaliyofanywa katika kanuni ndogo (2) atatoa kibali cha utalii wa uwindaji kwa mwombaji kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 43 cha Sheria.

(4) Mkurugenzi kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3) anaweza kutoa kibali mwombaji kama iliyoainishwa katika Jedwali la Sita.

(5) Muda na ada ya kibali cha utalii wa uwindaji itakuwa kama ilivyoelezwa kwenye kifurushi cha safari kilichoainishwa katika Sehemu B ya Jedwali la Nne.

(6) Bila kujali kanuni ndogo ya (5), Mkurugenzi kabla ya muda wa maombi kuisha anaweza kuongeza muda usiozidi siku thelathini.

(7) Kibali cha uwindaji kilichotolewa chini ya kanuni hii-

(a) hakitahamishika kwenda kwa kampuni nyingine; na

(b) kitatumika katika kitalu husika kinachomilikiwa na kampuni yenye kibali hicho.

(8) Mtu yeyote ambaye atawasilisha taarifa za uongo wakati wa kuomba kibali au leseni, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi milioni tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitatu au vyote.

Mtazamaji

15. Mwindaji wa kitalii anaweza kuambatana na mtazamaji iwapo atalipa ada ya mtazamaji kama ilivyoainishwa katika Sehemu F ya Jedwali la Nne:

Isipokuwa kwamba, mtazamaji mwenye umri chini ya miaka kumi na nane anatakiwa kuambatana na mzazi au mlezi wake.

Masharti ya utalii wa uwindaji

16.-(1) Uwindaji utafanyika kati ya muda wa mawio na machweo.

(2) Kampuni ya uwindaji itafanya shughuli za uwindaji ndani ya kitalu cha uwindaji ilichopewa kwa kipindi cha umiliki kilichoainishwa katika Cheti cha Kupewa Kitalu cha Uwindaji na Mkataba husika.

(3) Bila kujali kanuni ndogo (2), Mkurugenzi anaweza-

(a) baada ya malipo ya ada iliyoainishwa katika Sehemu D ya Jedwali la Nne, kuidhinisha makubaliano ya kufanya uwindaji baina ya makampuni na kutoa kibali cha uwindaji kwa makampuni husika kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Sita kwa kuzingatia kwamba uwindaji huo ni kwa madhumuni ya-
   - (i) kumwezesha mteja wa uwindaji kupata spishi zisizopatikana katika kitalu cha uwindaji alichopewa;
   - (ii) kutatua vikwazo vya ratiba katika kitalu cha uwindaji husika;
   - (iii) kuongeza thamani ya nyara;

(b) kutoa kibali cha uwindaji wa ndege kwa kampuni ya uwindaji kwenye maeneo yanayomilikiwa na watu binafsi, baada ya kampuni hiyo-
   - (i) kuthibitisha umiliki wa ardhi na kulipa ada ya kibali cha kuwinda ndege kama ilivyoainishwa katika Sehemu B ya Jedwali la Nne; au
   - (ii) kuwasilisha kwa Mkurugenzi nakala ya hati ya makubaliano kati ya kampuni na mmiliki wa ardhi, ikiwa kampuni hiyo sio mmiliki wa ardhi husika na kulipa ada ya kibali cha kuwinda ndege kama ilivyoainishwa katika Sehemu B ya Jedwali la Nne:

Isipokuwa kwamba kibali cha uwindaji wa ndege kinachotolewa chini ya kanuni ndogo ya 3(b) kitatolewa katika umbali usiopungua kilomita moja kutoka

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

maeneo ya makazi ya watu.

(4) Kampuni ya uwindaji itahakikisha kwamba watu walioidhinishwa na Mkurugenzi pekee wanashiriki katika shughuli za uwindaji wakati wa kifurushi cha safari chochote.

(5) Mtu hataruhusiwa kuingia au kukaa katika kitalu cha uwindaji bila idhini ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi.

(6) Mkurugenzi au Jumuiya iliyoidhinishwa itahakikisha mwindaji wa kitalii anaambatana na afisa aliyeidhinishwa wakati wa shughuli za uwindaji.

(7) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (6), mwindaji wa kitalii ambaye hana leseni ya mwindaji bingwa chini ya Kanuni hizi, ataambatana na mwindaji bingwa mwenye leseni ipasavyo.

(8) Mwindaji bingwa anapaswa-

(a) mara baada ya kuwinda au kujeruhi mnyamapori kujaza na kusaini rejista iliyoainishwa katika Jedwali la Saba;

(b) kujaza fomu ya kurudi safari ya kuwinda simba iliyoainishwa katika Jedwali la Nane; na

(c) kuhakikisha fomu katika kipengele (a) na (b) zimejazwa, kusainiwa na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi.

(9) Kwa madhumuni ya kanuni hii "uwindaji baina ya makampuni" maana yake ni kampuni moja ya uwindaji kufanya uwindaji katika kitalu cha uwindaji kinachomilikiwa na kampuni nyingine.

Ombi la kufutwa kibali cha uwindaji

17.-(1) Kampuni ya utalii wa uwindaji inaweza wakati wowote kabla ya tarehe ya kuanza safari ya uwindaji kuwasilisha kwa maandishi maombi ya kufutwa kwa kibali cha uwindaji kwa Mkurugenzi.

(2) Mkurugenzi anaweza mara baada ya kupokea maombi ya maandishi kutoka kampuni ya uwindaji na kabla ya tarehe ya kuanza safari ya uwindaji kufuta kibali cha uwindaji ikiwa-

(a) kuna uthibitisho wa kufutwa kwa safari ya uwindaji kutoka kwa mwindaji; na

(b) asilimia kumi na tano ya ada iliyolipwa itabakia kama ada ya kufuta kibali na kiasi kilichobakia kitatumika kulipia ada zingine zilizoainishwa chini ya Kanuni hizi kadri kampuni ya uwindaji itakavyoelekeza.

Kibali kitakacho rejeshwa

18.-(1) Kampuni iliyopewa kibali cha uwindaji chini ya Kanuni hizi, ndani ya siku thelathini baada ya kuisha kwa muda wa matumizi ya kibali cha uwindaji, itarejesha kibali kwa Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa kinachoambatana na orodha ya wanyamapori waliowindwa na nyara kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tisa.

(2) Kampuni ya Uwindaji itakayoshindwa kuzingatia kanuni ndogo (1), itatakiwa kulipa malipo ya ziada ya asilimia tano ya ada ya kibali.

Ada ya mnyamapori

19.-(1) Kampuni ya uwindaji, ndani ya siku ishirini na nane baada ya kutolewa kwa ankara na namba ya malipo, italipa ada ya mnyamapori kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi.

(2) Kampuni ya uwindaji itakayoshindwa kulipa ada ya mnyama iliyoainishwa katika kanuni hii, itatakiwa kulipa tozo ya asilimia tano ya ada ya mnyama.

(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (2) Mkurugenzi hatashughulikia maombi ya kibali cha uwindaji kwa kampuni ya uwindaji iliyoshindwa kulipa ada ya wanyamapori ndani ya siku thelathini.

(4) Baada ya malipo ya ada ya wanyamapori, Mkurugenzi atasajili nyara na kutoa cheti cha umiliki wa nyara.

(5) Mkurugenzi atataifisha nyara ikiwa kampuni itashindwa kuendana na masharti ya Kanuni hizi.

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

Matumizi na udhibiti wa mgao wa wanyamapori

20.-(1) Kampuni ya uwindaji iliyopewa kitalu cha uwindaji itatumia angalau asilimia 40 ya wanyamapori maalum walioainishwa katika Jedwali la Kumi na Moja katika mgao wake wa wanyamapori iliyopewa katika kitalu husika.

(2) Endapo kampuni ya uwindaji itashindwa kukidhi matakwa ya kanuni ndogo ya (1) itatakiwa kulipa tofauti ya asilimia 40 ya ada ya wanyamapori maalum.

(3) Endapo kampuni ya uwindaji haijatumia kabisa mgao wake wa wanyamapori itatakiwa kulipa asilimia 100 ya thamani ya mgao wa wanyamapori maalum.

Mchango kwa jamii

21.-(1) Mmiliki wa cheti cha kitalu cha uwindaji, kila mwaka, atalipa kiasi kisichopungua milioni kumi na tatu na laki tatu kwa Mkurugenzi kama mchango wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii.

(2) Kiasi kilichoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitalipwa kwa Mkurugenzi kila mwaka kabla au tarehe ya kupewa kitalu cha uwindaji.

(3) Kampuni ya uwindaji ambayo itashindwa kulipa mchango kwa jamii kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) itatakiwa kulipa mchango wa jamii pamoja na malipo ya ziada ya asilimia 5 ya malipo ya mchango kwa jamii.

Tathmini ya utendaji wa kampuni ya uwindaji

22.-(1) Kutakuwa na tathmini ya utendaji kwa kila mwaka kwa kampuni ya uwindaji iliyopewa kitalu cha uwindaji itakayozingatia vigezo vifuatavyo:

(a) kukidhi matakwa ya matumizi ya mgao wa wanyamapori kwa mujibu wa kanuni ya 20;
(b) uchangiaji katika uboreshaji wa miundombinu na ulinzi wa mazingira ndani ya kitalu chake cha uwindaji;
(c) uchangiaji katika oparesheni za kuzuia ujangili au kupambana na shughuli nyingine yoyote haramu inayohusu uhifadhi wa wanyamapori;
(d) uwepo wa kumbukumbu za kampuni kuhusiana na usafirishaji wa nyara nje ya nchi;
(e) kukidhi matakwa ya uchangiaji wa miradi ya jamii;
(f) ulipaji wa ada za kitalu kwa wakati na tozo nyingine zilizoainishwa kisheria; na
(g) uzingatiaji wa Sheria na Kanuni hizi.

(2) Tathmini ya utendaji ya mwaka iliyorejewa katika kanuni ndogo (1), itafanywa na-

(a) Mkurugenzi kwa kampuni za uwindaji chini ya Kanuni hizi; na
(b) Mkurugenzi kwa kampuni za uwindaji zilizopewa kitalu katika maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori.

(3) Taarifa ya tathmini ya utendaji ya mwaka itawasilishwa kwa Waziri kwa ajili ya-

(a) tathmini ya jumla ya utendaji wa kampuni ya uwindaji; na
(b) maamuzi ya muendelezo wa kipindi cha umiliki.

Masharti ya kuhamisha kitalu cha uwindaji

23.-(1) Kampuni ya uwindaji haitahamisha haki ya matumizi ya kitalu cha uwindaji iliyopewa, isipokuwa kama kampuni hiyo imepata ridhaa ya maandishi ya Waziri.

(2) Kampuni ya uwindaji inayotarajia kuhamisha kitalu cha uwindaji itamjulisha Mkurugenzi kwa maandishi.

(3) Taarifa iliyoainishwa chini ya kanuni ndogo (2) itaambatishwa na-

(a) uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya kuhamisha kitalu kama ilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Nne;
(b) taarifa za kina za kampuni inayotarajiwa kuhamishiwa kitalu cha uwindaji;

(c) uthibitisho wa malipo ya tozo zote zilizoainishwa;
(d) cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi kwa kila kampuni; na
(e) makubaliano yote ya uhamishaji wa kitalu cha uwindaji.

(4) Mkurugenzi baada ya kupokea maombi ya kuhamisha kitalu cha uwindaji kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2) na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, atafanya uhakiki wa kampuni inayokusudiwa kuhamishiwa kitalu.

(5) Mkurugenzi baada ya kufanya uhakiki wa maombi ya kuhamisha kitalu cha uwindaji, atawasilisha taarifa ya uhakiki na mapendekezo yake kwa Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji kwa ajili ya mapitio na kumshauri Waziri.

(6) Waziri kwa kuzingatia ushauri chini ya kanuni ndogo ya (5) anaweza kukubali au kukataa maombi ya kuhamisha kitalu.

(7) Waziri akiridhia ombi la uhamishaji wa kitalu, atatoa cheti cha Kugawa Kitalu cha Uwindaji kwa kipindi kilichobaki kwa kampuni ya uwindaji kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

(a) malipo ya ada ya kuhamisha kitalu kama ilivyoainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Nne;
(b) uwasilishwaji wa makubaliano yaliyosainiwa ya uhamishaji wa kitalu cha uwindaji; na
(c) atarejesha cheti cha kupewa kitalu cha uwindaji.

(7) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "kuhamisha kitalu cha uwindaji" maana yake ni kuhamisha haki ya matumizi ya kitalu cha uwindaji kutoka kampuni moja kwenda kwa anayehamishiwa na inajumuisha mazingira ambayo hisa zilizo nyingi katika kampuni ya uwindaji zinahamishwa kwenda kwa mtu mwingine.

(8) Kampuni ya uwindaji ambayo itakiuka kanuni hii inatenda kosa na ikitiwa hatiani itawajibika kwa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi milioni kumi.

**Kurejesha kitalu cha uwindaji**

24.-(1) Kampuni ya uwindaji inayotarajia kurejesha kitalu cha uwindaji kabla wa matumizi yake kuisha itatoa notisi ya maandishi ya kurejesha kitalu kwa Waziri miezi mitatu kabla tarehe ya kufanya malipo ya ada ya kitalu.

(2) Waziri, ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya kupokea notisi-

(a) ataridhia maombi ya kurejeshwa kwa kitalu cha uwindaji kwa kuzingatia kwamba kampuni ya uwindaji imelipa madeni yote inayodaiwa; na
(b) atatoa barua ya kuridhia ombi la urejeshwaji wa kitalu.

(3) Kampuni ya uwindaji itakayoshindwa kukidhi masharti ya kanuni ndogo (1) itawajibika kulipa ada ya kitalu cha uwindaji kwa mwaka husika.

**Kufutwa kwa umiliki**

25. Waziri anaweza muda wowote kabla ya kumalizika kwa muda wa uwindaji, kufuta umiliki wa kitalu cha uwindaji ikiwa kuna ushahidi wa kutosha kwamba mtu aliyepewa kitalu cha uwindaji-

(a) ameshindwa kukamilisha suala au muunganiko wa masuala yanayotakiwa kuzingatiwa na Waziri;
(b) alitoa taarifa za uongo au zisio sahihi kwenye maombi ya kitalu cha uwindaji;
(c) amekutwa na hatia ya kosa chini ya Sheria;
(d) ameshindwa kulipa ada za lazima au madeni mengine anayotakiwa kulipa kuhusiana na kitalu cha uwindaji;
(e) amekodisha kitalu cha uwindaji alichopewa; au
(f) amehamisha kitalu cha uwindaji kinyume na Kanuni hizi.

**Mamlaka ya afisa mwidhiniwa**

26. Afisa mwidhiniwa muda wowote anaweza kuingia kitalu cha uwindaji chochote kwa madhumuni ya kutekeleza jukumu lake lolote au kutekeleza mamlaka au hadhi aliyopewa chini ya Sheria.

**Leseni ya**

27.-(1) Mtu hatamwongoza mteja wa uwindaji wakati wa safari ya uwindaji

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

mwindaji bingwa

isipokuwa kama ana leseni ya mwindaji bingwa iliyotolewa na Mkurugenzi chini ya Kanuni hizi.

(2) Mtu yeyote anayetarajia kuwa mwindaji bingwa atawasilisha maombi rasmi kwa Mkurugenzi kwa kujaza Fomu iliyoanishwa katika Jedwali la Kumi na Mbili.

(3) Mkurugenzi kabla ya kutoa cheti cha mwindaji bingwa, atahakikisha kwamba mwombaji ana-

(a) sifa zilizoainishwa chini ya Sheria;
(b) amefaulu mtihani wa mwindaji bingwa wa daraja aliloomba; na
(c) amelipa ada ya mwindaji bingwa kama ilivyoainishwa katika Sehemu C ya Jedwali la Nne.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya 3(b) Mkurugenzi atateua timu kwa ajili kutahini waombaji wa uwindaji bingwa.

(5) Mkurugenzi baada ya kujiridhisha kwamba mwombaji amekidhi matakwa yaliyoainishwa chini ya kanuni hii, atatoa leseni ya mwindaji bingwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Tatu.

(6) Leseni ya mwindaji bingwa itakuwa halali kwa miaka miwili na itakuwa katika madaraja yafuatayo:

(a) Daraja A ambalo litamruhusu mmiliki kusimamia uwindaji wa wanyama wote; na
(b) Daraja B ambalo litamruhusu mmiliki kusimamia uwindaji wa wanyama wasio hatari.

(7) Mwindaji bingwa ataruhusiwa kuwaongoza wawindaji wasio zidi wawili ndani ya safari ya uwindaji:

(8) Isipo kuwa kwamba, kwa mwindaji wa ndege au uvuvi wa michezo mwindaji bingwa anawezakusimamia wawindaji waiozidi wa nne.

(9) Mkurugenzi anaweza kufuta leseni ya mwindaji bingwa na kumzuia kufanya maombi ya leseni nyingine kwa kipindi cha miaka mitatu endapo atajiridhisha mwindaji bingwa-

(a) ametoa taarifa za uongo ili kupata leseni hiyo; au
(b) ametenda kosa chini ya Sheria.

Usafirishaji wa nyara nje ya nchi

28.-(1) Kampuni ya uwindaji itasafirisha nje ya nchi nyara zote zilizowindwa na zitakazoitajika kusafirishwa ndani ya msimu wa uwindaji na ndani ya miezi kumi na nane baada ya msimu wa uwindaji kuisha.

(2) Ikiwa kampuni ya uwindaji inashindwa kusafirisha nyara chini ya kanuni ndogo ya (1), itatakiwa kutoa taarifa ya hali ya nyara kwa Mkurugenzi kila robo mwaka.

(3) Endapo kampuni ya uwindaji inashindwa kutoa taarifa kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo (2) kwa robo mwaka tatu mfululizo itatakiwa kulipa malipo ya ziada ya 5% ya thamani ya nyara zilizowindwa.

(4) Mwindaji anayetarajia kuhamisha umiliki wa nyara kwa madhumuni ya kusafirisha kwenda nje ya nchi kwa mwindaji au kampuni nyingine atatakiwa kulipa ada ya maombi ya kuhamisha kiasi cha shilingi za kitanzania laki sita.

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

## SEHEMU NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Kosa la kukiuka kiwango kilichowekwa

29.-(1) Mkurugenzi ataweka viwango vya ubora na ukubwa wa nyara za utalii wa uwindaji.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo (1), mtu hatawinda-

(a) tembo ambaye jino lake moja lina uzito chini ya kilogramu 20 au lina urefu chini ya sentimita. 160;

(b) chui ambaye urefu wake kuanzia kweye ncha ya pua hadi mwisho wa mkia ni chini ya sentimita. 130; na

(c) mamba ambaye urefu wake kuanzia ncha ya pua hadi ncha ya mkia ni chini ya sentimita. 300.

(3) Mwindaji bingwa yeyote ambaye anamwongoza mteja kuwinda kwa kukiuka masharti ya kanuni hii anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi milioni tano.

(4) Mtu atakayewinda simba mwenye umri chini ya miaka sita anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika-

(a) ikiwa simba anayewindwa ana umri wa miaka minne au mitano, faini ya shilingi milioni tano na atarauhusiwa kusafirisha nyara nje ya nchi;

(b) ikiwa simba aliyewindwa ni chini ya umri wa miaka minne-

(i) kulipa faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya kwanza ya utendaji wa kosa;

(ii) kulipa faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya pili ya utendaji wa kosa; au

(iii) kulipa faini ya shilingi milioni tano kwa mara ya tatu ya utendaji wa kosa.

(5) Ikiwa simba aliyewindwa ni chini ya umri wa miaka minne, Mkurugenzi atatoza faini iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (4) na atataifisha nyara iliyowindwa.

(6) Mkurugenzi anaweza kusimamisha leseni ya mwindaji bingwa kwa kipindi cha miaka mitatu endapo atajiridhisha mwindaji bingwa amekiuka masharti ya Kanuni hizi kwa kutenda kosa mara tatu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Adhabu ya jumla

30. Mtu ambaye anakiuka masharti ya Kanuni hizi ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyoainishwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi milioni tano au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka mitano au vyote kwa pamoja.

Rufaa

31.-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mkurugenzi chini ya Kanuni hizi atawasilisha rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini kuanzia siku ya uamuzi.

(2) Waziri baada ya kupokea rufaa iliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo (1) atatoa uamuzi ndani ya siku arobaini na tano.

Kufutwa

32.-(1) [Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2015 zimefutwa.]

(2) Bila kujali kufutwa kulikofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitu chochote kilichofanyika au kitendo kilichotokea au kinachochukuliwa kufanyika au kibali, cheti, leseni yoyote chini ya kanuni zinazofutwa itachukuliwa kufanyika au kutolewa, kadri itakavyokuwa chini ya masharti ya Kanuni hizi.

TS Na. 414 la 2015

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

**JEDWALI LA KWANZA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

CHETI CHA UGAWAJI WA KITALU CHA UWINDAJI
*(Limetengenezwa chini ya kanuni 3(1))*

Sehemu kilipotolewa :……………………..…………………………………………………………………..
Tarehe ya kutolewa :……………………..………………………………..……………………………………….
Tarehe ya kumaliza muda wa matumizi (inategemea uzingatiaji wa kanuni)
……….……………………….
Imetolewa kwa:
…………………………………………………..……………………………………………….
Jina la kampuni na anuani:
……………………………………..……………………………
Maelezo ya mipaka ya kitalu cha uwndaji
……………………………………………………………………..………………………..………………………………
…………………
……………………..……………………….……………………………………………………………………...……
……………………..…

Masharti maalum yanayoambatana na kitalu au vitalu vya uwindaji
……………………………………………………………..……………………………………..
……………………………………………………………..………………………
Saini ya Waziri na mhuri wa ofisi

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1))*

A. MAELEZO YA VIGEZO KWA AJILI YA KUTENGA MADARAJA YA VITALU VYA UWINDAJI

| **Alama / Vigezo** | **A** | **B** | **C** | **D** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **4** | **3** | **2** | **1** | **Uzito** |
| Aina za spishi | Juu | Kati | Chache | Hakuna | 5 |
| Ndani ya Pori la Akiba (GR) na karibu na Hifadhi ya Taifa (NP) au Eneo la Mamlaka ya Ngorongoro (NCA) | Kinapakana na hifadhi ya taifa na/au eneo la Mamlaka ya Ngorongoro | Ndani ya GR au kinapakana na/au vitalu vingine vya uwindaji | Kinapakana na GR lakini haijazungukwa na GR | Imesimama peke yake na/ au kitalu kilichojitenga | 5 |
| Kuenea kwa makazi | Aina kuu 4 | Aina kuu 3 | Aina kuu 2 | Aina kuu 1 | 4 |
| Umbali kutoka kiwanja cha ndege kilicho jirani | Ndani ya kitalu | < km 20 | km 20 – 40 | > km 40 | 2 |
| Umbali kutoka kitalu hadi majiji ya kuingilia au kutokea; Dar es Salaam na Arusha | Ndani ya km 300 km | km 300-600 | km 600- 1000 | > km 1000 | 2 |
| Kufikika kwa barabara – umbali hadi barabara kuu iliyojirani | Inagusa kitalu au inakatisha kitalu | Si zaidi ya km 20 | km 20-50 | > km 50 | 3 |
| Maji ya wanyamapori | Mengi ya kudumu na msimu | Chanzo kimoja cha kudumu | Msimu pekee | Hakuna | 4 |
| Shughuli za kibinadamu | <10% | 10-20% | 21-50% | >50% | 4 |
| Wingi wa spishi zinazowindwa ikilinganishwa na bei ya leseni katika TZS | >41 thamani iliyopangwa | 38-41 | 33-37 | <33 | 4 |
| Wingi wa spishi zinazowindwa ikilinganishwa na thamani ya siku za safari | > 113 | 100-113 | 85-99 | <85 | 3 |

GPA = Jumla ya Wastani wa Alama ÷ Jumla ya Uzito (= 105 ÷ 34 = 3.088)

Kumbuka: Alama za Daraja = (uzito wa kigezo) X (alama za kigezo cha kitalu)
Thamani ya kitalu A = 4, B= 3, C = 2 and D = 1

B. ALAMA ZA GPA KWA AJILI YA MADARAYA VYA VITALU VYA UWINDAJI

*(Zimejikita katika umbali sawa katika uwiano wa kiwango cha chini na cha juu wa alamaB)*

| **Daraja** | **Kiwango cha juu cha GPA** | **Kiwango cha chini cha GPA** |
|---|---|---|
| I | 3.6 | 3.1 |
| II | 3.0 | 2.4 |
| III | 2.3 | 1.7 |

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

**JEDWALI LA TATU**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni za 8(2) na 9(4))*

FOMU YA MAOMBI YA KITALU CHA UWINDAJI

1. Jina la kampuni: ………………………………………………….………………………………………
2. (a) Anuani ya Eneo Kuu la biashara: ……………………………………………………………………..

3. (b) Anuani ya posta:
………………………………………………………………..……………………………………
(c) Namba ya simu: …………………………………………………...………………………………
(d) Namba ya faksi: ………………………………………………………………….……………………
(e) Baruapepe: …………………..………….. Tovuti: ………..………….…………………………………………
(f) Linakopatikana eneo lingine *(eleza kama unalimiliki au umekodisha na hadhi yake kama ni ofisi, gereji, stoo nk.:*
……………………………………………………………

4. Majina kamili ya mmiliki (wamiliki) au mwanahisa (wanahisa) wa Kampuni na asilimia zao za hisa:
……………………………………………………...………………………………
……………………………………………………...………………………………
……………………………………………………...………………………………
……………………………………………………...………………………………
5. Umri, nchi ya kuzaliwa na utaifa wa sasa (wa watu waliotajwa katika namba 4 hapo juu):
..........................................................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................................................
..............................................................................................
6. Majina kamili ya Wakurugenzi wa Kampuni na taaluma zao:
..........................................................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................................................
..........................................................................................................................................................................................
..............................................................................................
7. Jina, sifa, uzoefu na utaifa wa wawindaji bingwa wenye ajira za kudumu:
*(Ambatisha karatasi nyingine kutoa maelezo hapo juu)*
8. Maelezo ya kitalu/vitalu vya uwindaji unavyoomba:

| **Na.** | **Jina la kitalu cha uwindaji** | **Daraja** | **Eneo la kijiografia** | **Uzoefu ndani ya Tanzania au mahali pengine** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mapato ya moja kwa moja kwa TAWA | Kodi iliyolipwa TRA |
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |

9. Orodhesha taarifa za magari na vifaa ulivyonunua au uthibitisho wa uwezo wa kifedha kupata vifaa vyote muhimu na zana kwa madhumuni ya kuendesha uwindaji.
…………………………………...……………………………………………………
10. Onesha chanzo chako na wingi wa wateja wako:
…………………………...………………………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 780 (Linaendelea)*

